

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Saba – Tarehe 13 Aprili, 2017

(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Saba, leo pia ni Kikao cha Saba. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Menejimenji ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Ripoti ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Fedha za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2016 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General*

on the Financial Statement of the Local Governments for the year ended 30th June 2016).

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Udhibiti wa Uendelezaji wa Maeneo ya Wazi Yaliyoainishwa nchini Tanzania (*Performance Audit Report on the Enforcement of Development Control for the Planned Public Open Spaces in Tanzania*).

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Miundombinu ya Shule za Msingi Tanzania (*Performance Audit Report on the Availability and upkeeping of Primary Schools' Infrastructure in Tanzania*).

Taarifa ya Majibu ya Serikali na Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Ripoti ya mwaka ya Ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016 (*The Annual Audit General Report of the Controller and Auditor General on the Financial Statements of the Central Government for the year ended 30th June, 2016*).

Ripoti ya mwaka ya Ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016 (*The Annual Audit General Report of the Controller and Auditor General on the Financial Statements of Development Projects for the year ended 30th June, 2016*).

Ripoti ya mwaka ya Ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za fedha za Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016 (*The Annual Audit General Report of the*

Controller and Auditor General on the Financial Statements of Public Authorities for the year ended 30th June, 2016).

Ripoti ya Jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalum kwa kipindi kinachosihia tarehe 31 Machi, 2017 (*The Annual Audit General Report of The Controller and Auditor General on Performance and Specialised Audit for the Period ending 31st March, 2017).*

Ripoti ya Ukaguzi na Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi katika Taarifa Tano za Ukaguzi wa Ufanisi zilizotolewa na kusomwa Bungeni kuanzia mwaka 2012 hadi 2013 (*Follow up Report on the Implementation of the Controller and Auditor General's Recommendations for the Five Performance Audit Reports Issued and Tabled to Parliament between 2012 and 2013).*

Majibu ya Hoja na Mpango wa kutekeleza Mapendekezo ya Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha 2015/2016 *Volume II* na *II* (A na B).

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Uzalishaji wa Wahitimu katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia (*Performance Audit Report on the Produced Graduates in Oil and Natural Gas Industry).*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Usalama Dhidi ya Moto katika Majengo ya Umma. (*Performance Audit Report on the Enforcement of Fire Safety in Public Buildings).*

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Samani za Barabarani (*Performance Audit Report on the Management of Roads Furniture*).

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Kaguzi za Vyombo vya Majini kwa ajili ya kupewa Vyeti vya Ubora na Kukidhi Viwango vya Usalama wa Usafirishaji (*Performance Audit Report on the Management of Surveys and Inspections of Vessels in the Maritime Transportation*).

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Uchukuaji wa Maji kutoka Vyanzo vya Maji (*Performance Audit Report on the Control of Water Abstraction from the Water Sources*).

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Mikataba iliyoingwiwa kati ya Serikali na Hospitali za Binafsi Nchini. (*Performance Audit Report on the Management of Hospital Agreements Between the Government and Private Hospitals*).

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali ya kawaida. Tunaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kabla ya kumruhusu Mheshimiwa mhusika kuuliza swali, niwape tu taarifa ya kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo, yupo kikazi nje

ya Dodoma na badala yake anayekaimu shughuli hizo hapa Bungeni kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni ni Mheshimiwa Waziri Dkt. Hussein Mwinyi. (*Makofi*)

Sasa namruhusu Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege Mbunge wa Kalambo atuulizie swali lake.

Na. 55

Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi Dar Es Salaam

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE aliuliza:-

Serikali ilipata mkopo kutoka Benki ya Dunia na kujenga miundombinu ya mradi wa mabasi yaendayo kasi Jijini Dar es Salaam. Baada ya ujenzi wa mradi huo kukamilika Serikali ilitoa msamaha wa baadhi ya kodi wakati wa uingizaji nchini mabasi yanayotumika kusafirisha abiria katika mradi huo. Serikali inamiliki asilimia 49 ya hisa za mradi huo na mwekezaji asilimia 51.

(a) Wakati wa kukokotoa hisa kati ya Serikali na mwekezaji, je, sehemu ya msamaha imejumlishwa katika ukokotoaji wa hisa?

(b) Je, ni nini faida na hasara za msamaha huo wa kodi upande wa Serikali?

(c) Wakati wa kulipa mkopo huo, je, ni nini wajibu wa mwekezaji katika mkopo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kimsingi mwekezaji hakupata msamaha wa kodi wakati wa kuingiza mabasi nchini bali alipewa punguzo la kodi hiyo (*import duty*) kutoka asilimia 25 inayotozwa hadi asilimia 10. Punguzo hilo lilitolewa kwa makubaliano na nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(b) Mheshimiwa Spika, punguzo la kodi hiyo limesaidia kutoa unafuu wa nauli zinazotozwa kwa abiria wanaotumia mabasi ya *UDART*. Endapo punguzo hilo lisingekuwepo ni dhahiri kwamba gharama hizo zingejumuishwa katika viwango vya nauli kwa watumiaji.

(c) Mheshimiwa Spika, mwekezaji anawajibika kurejesha mkopo aliochukua kwa ajili ya kununulia mabasi pamoja na kulipa kodi Serikalini kwa mujibu wa sheria za nchi. Kwa upande wake, Serikali inawajibika kulipa mkopo Benki ya Dunia ambao ulitumika kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa *DART* awamu ya kwanza kwa kuzingatia makubaliano (*financing agreement*).

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wakati naandika swali hili, nilitaka lijibiwe na Wizara ya Fedha na si kwamba nilikuwa nimekosea kwa kuitaka Wizara ya Fedha ijibu swali hilo.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika na Serikali wanakiri pale ambapo mwekezaji unampunguzia badala ya kulipa asilimia 25 akalipa asilimia 10 maana yake hiyo ni pesa ambayo ingeweza kwenda kwa Watanzania, ni *tax* ambayo ilitakiwa kuwa imekusanywa, haikukusanywa.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, je, isingekuwa busara nafasi hiyo inekuwa imetolewa kwa Mtanzania awae yeyote ambaye ananunua mabasi ya aina hiyo *either* anapeleka Mwanza, anapeleka Sumbawanga akaweza kupata fursa kama hiyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, katika utaratibu wa Serikali kujenga barabara hizi kwa awamu ya kwanza ambayo imeshakamilika sasa tunaenda awamu ya pili na mpak aya tatu, ni wazi kwamba Serikali itaendelea kuwekeza na katika hali ya kawaida ili muweze kugawana lazima kila mmoja aoneshe rasilimali ambayo amewekeza. Je, ni busara kwamba pamoja na uwekezaji ambao utaendelea kuwekwa na Serikali, bado mwekezaji huyu aendelee kumiliki asilimia 51 na Serikali ibaki na asilimia 49? (*Makofi*)

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Simbachawene.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri Mheshimiwa Jafo, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kandege kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tufahamu kwamba mradi huu kwa *nature* yake ni PPP ni *Public Private Partnership* na kwa sababu ni PPP na kusema ukweli sisi hatuna uzoefu mkubwa sana wa miradi ya PPP hapa nchini, lakini PPP hii ni PPP ambayo kusema ukweli inagusa *the public direct*, kwa maana ya usafiri wa wananchi wa Dar es Salaam lakini PPP hii ni PPP ambayo inawahusisha kampuni ya Kitanzania na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la misamaha ni kweli jambo limekuwa likipigiwa kelele kuhusu misamaha. Ipo misamaha mingi imetolewa na Bunge limekuwa likisema juu ya suala la misamaha. Lakini huu ni msamaha wa aina yake, tena ni kwa eneo ambalo linaleta unafuu kwa wananchi hao hao. Sasa mimi nimuombe tu Mheshimiwa Kandege aje tumpe *details* zaidi za suala hili. Pengine swali hili aliliuliza muda mrefu uliopita kwa hiyo limeshabadilika sana na tumekwenda mbali zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ameuliza je, katika mwendelezo wa hatua zingine zinazofuata za uendelezaji

wa mradi huu, umiliki wa kampuni hii binafsi na Serikali utabakia asilimia ile ile?

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema tu kwamba katika hiyo asilimia 51 na asilimia 49 ni katika mradi huu wa awamu hii kwa sababu ni kampuni inayoundwa na Serikali kwa maana ya *Simon Group* na Serikali wameunda kampuni inayo-*operate* mabasi haya ya *UDART* ambayo yanafanya usafiri Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo unaona Serikali katika kila hatua imo na ndiyo maana tusipokuwa makini na jambo hili sio watu wote wanalipenda na hasa wenzetu. Kwa hiyo, ninaposema wenzetu sina maana upande wowote wa Bunge hapana, nina maana nje kwasababu wangependa *PPP* ya aina fulani. Nadhani mmenielewa.

Kwa hiyo, niwasihi sana Waheshimiwa Wabunge, hii ni *PPP* nzuri ambayo kila kitu kinabaki hapa hapa ingelikuwa ni kampuni imetoka Bogota imetoka wapi, hapo ndio lakini hii ni *PPP* nzuri na ninaomba sana kama Jiji waliuza hizi asilimia 51 na Serikali tumeweza ku-*acquire*, kwanza ilikuwa zaidi ya hapo; tumeweza ku-*acquire back* karibu hizi 49%. Tuendeleo lakini ni kwa hatua ya awamu hii tu ndiyo wameshinda hii *tenderya* kuendesha hii na awamu zinazofuata na zenyewe zitakuwa *procured* kwa utaratibu mwingine.

SPIKA: Ahsante sana. Nimekuona Mheshimiwa Abdallah Mtolea kwa upande wa CUF, halafu kwa upande wa CHADEMA utauliza swali la mwisho la nyongeza.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa suala la usafiri Jijini Dar es Salaam hasa *public transport* ni jambo nyeti na linawagusa wananchi wote kwa ujumla wao; kwa mazoea katika Majiji ya wenzetu Ofisi za Mameya zinahusika sana katika kusimamia usafiri katika Majiji yao. Kwa mfano katika Jiji la London Ofisi ya Meya wa Jiji la London inahusika mpaka kupanga ratiba za treni, ratiba za mabasi na *route* zenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilitaka kujua kwanini katika Jiji la Dar es Salaam Ofisi ya Meya haihusishwi kwa namna yoyote katika upangaji wa *route* au kusimamia usafiri katika Jiji la Dae es Salaam?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimwa Spika, ni kweli huo ndiyo utaratibu wa Majiji mengi, lakini tatizo letu hapa ni historia ya UDA na Jiji la Dar es Salaam. Jiji la Dar es Salaam waliziuza hizi hisa kwa Kampuni ya *Simon Group*. Tumejaribu kutafuta namna ya kusaidia, ni Serikali Kuu ndio tuliojitahidi kurudisha asilimia 49 za kwetu maana za zenyewe zilitaka kupotolea huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na kusema ukweli nimpongeze sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika jambo hili tumeshirikiana vizuri. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa *guidance* zake mpaka tumeweza hata hizo asilimia 49 zenyewe zilikuwa ni kiini macho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini Waheshimiwa Wabunge tukumbuke pia historia ya UDA ilivyokuwa, kilikuwa ni kitu ambacho kimetupwa, kimeachwa huko lakini baadaye kimerudi na kuwa kitu chenye thamani leo ndiyo tunasema. Waulize wao Jiji la Dar es Salaam wapo, wamewahi kwenda hata Mahakamani kudai kwamba uuzaji huu sio halali? Na kama walikwenda je, ilikuwaje? Na matokeo ya kesi yalikuwaje, mbona sasa hawasemi kwamba tunataka ku-*appeal*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe sana, Jiji la Dar es Salaam *is a legal entity*. Wao wanaweza kushtaki na kushtakiwa, wasije hapa Bungeni, maana walipouziana hawakuleta hapa Bungeni tukapitisha. Waende wakatafute kama hawakuuza sawasawa waone wanavyoweza kufanya, lakini kwa sasa sisi kama Serikali Kuu tumeweza kurejesha asilimia 49 ya hisa zetu na zinaendeshwa kwenye mikono ya Serikali na tume-*win tender* ya ku-*operate* mabasi ya Dar es Salaam kwa kushirikiana na huyo mwekezaji binafsi. (*Makofi*)

SPIKA: Nilishakuruhusu Mheshimiwa swali la mwisho la nyongeza.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuuliza swali langu la nyongeza kwa rufusa yako naomba niweke rekodi sawasawa, kwamba hisa za Jiji la Dar es Salaam hazikuuzwa jana, ziliuzwa toka mwaka 2009 wakati sisi hatujawa katika uongozi wa Jiji la Dar es Salaam.

Kwa kuwa Waziri ameliambia Bunge kwamba ule mkataba wa uendeshaji wa usafirishaji wa Jiji la Dar es Salaam ni wa muda na kwamba wao *Simon Group* ndio wameshinda hiyo zabuni, lakini kwa kuwa mkopo uliojenga miundombinu ya barabara za Jiji za Dar es Salaam umetolewa na Benki ya Dunia, na kwa kuwa mkopo ulionunua magari yaendayo kasi Dar es Salaam umetolewa na Benki ya NMB, na Serikali ndiyo dhamana wa Benki hiyo haoni kwamba sio halali kwa mtu mmoja kumiliki uendeshaji wa mabasi yaendayo kasi Dar es Salaam na kuacha wananchi wengine ambao wana mabasi madogo madogo kuachwa nje ya utaratibu?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwanza *NMB* ni ya nani? Serikali tuna hisa kwenye *NMB*. Kwa hiyo hakuna hata dhambi yoyote kwa *NMB* ku-*facillitate*, maendeleo ya usafiri wa Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini zile *arrangement* za *NMB* na huyu mwekezaji ambaye anaendesha mradi wa mabasi yaendayo kasi Dar es Salaam ambaye ni Serikali na mwekezaji binafsi *it is a PPP*, ni mradi ambao una-*arrangements* zake. *Arrangements* zile ni za kati ya *UDART* ambayo Serikali imo na *Simon Group* na benki na ujenzi wa miundombinu ni makubaliano ya Serikali na *World Bank* wala utaratibu wa

uendeshaji haukuwa ni jambo muhimu sana, hapa ilikuwa ni kuboresha usafiri katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanafahamu adha ya foleni ya Dar es Salaam, Watanzania wanafahamu namna tunavyopoteza uchumi katika Jiji la Dar es Salaam, hivi kwa nini sisi Watanzani tuna-*tend* kuchukua PPP. Hatuwezi kujenga hii nchi kwa kutegemea Serikali peke yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda sana fikra za baadhi ya Wabunge, fikra za kuamini kwamba *private sector* ni muhimu katika ujenzi wa uchumi, na siogopi mimi kum-*quote* Mheshimiwa Zitto Kabwe kwamba ni mtu anayejua sana eneo hilo la uchumi. Lakini Waziri wa Fedha amekuwa akieleza hapa eneo hilo, lakini bado sisi Watanzania anaposhiriki mswahili katika shughuli yoyote ya PPP ni nongwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu haiwezi kuendelea kwa msingi huu, ila angekuja mgeni kutoka nje angeshangiliwa kweli kweli, kwani hamjui kwamba kuna hisa nyingi zinachukuliwa kwenye makampuni ambayo Serikali ilitakiwa kushiriki lakini tumeshindwa.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuendelea na msingi huu wa kuendesha uchumi na uchumi ukaenda kama mawazo yenyewe ndiyo haya.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu, imelinda maslahi yake na inafahamu mradi huu umuhimu zaidi si faida bali huduma kwa wananchi wa Dar es Salaam. (*Makofi*)

SPIKA: Kwa majibu hayo ya uhakika siruhusu tena swali lingine la nyongeza hapo. Tunaendelea, Mheshimiwa Waziri nimeipenda hiyo, angekuwa ni mtu wa kutoka majuu huko, lakini akishakuwa Mmatumbi basi tena. (*Kicheko*)

Tunaenda Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Salma Mohamed Mwassa, Mbunge wa Viti Maalum swali lako tafadhali.

Na. 56

Umuhimu wa Kurasimisha Ardhi

MHE. SALMA M. MWASSA aliuliza:-

Je, ni nini umuhimu wa kurasimisha ardhi kwenye maeneo ambayo hayajapimwa?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salma Mohamed Mwassa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, urasimishaji wa ardhi maana yake ni kutambua miliki za wananchi kwenye maeneo yaliyoendelezwa bila kupimwa kisheria. Matokeo ya urasimishaji ni kutoa hatimiliki na kuweka miundombinu ya msingi kama vile barabara, maji, mifereji ya maji ya mvua na ikiwezekana kuweka majina ya mitaa. Kwa kawaida, urasimishaji ni zoezi shirikishi limaloweza wananchi kukubaliana mipaka ya viwanja, kufungua njia na kutoa maeneo ya huduma za jamii kama vile shule, vituo vidogo vya polisi, makaburi, zahanati na maeneo ya wazi.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kurasimisha maeneo haya ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, urasimishaji unatoa fursa kwa wananchi kutumia ardhi kupitia nyaraka za umiliki wa ardhi kama vile hati, kuweka dhamana ya mikopo katika taasisi za fedha, mahakama.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuongeza thamani ya ardhi au nyumba husika (*value addition*) iwe kwa kuweka dhamana (*collateral*) rehani, upangishaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuboresha makazi hususan kwa kuweka miundombinu ya msingi ili kurahisisha usafiri, kupunguza madhara yatoakanayo na majanga mbalimbali kama vile mafuriko na moto. Kwa upana wake urasimishaji ni dhana inayochangia kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, nne ni kutoa uhakika wa milki ya ardhi na hivyo kuwa kivutio kwa mazingira ya uwekezaji. Kwa mfano, maeneo mengi ambayo yamerasimishwa, kumekuwa na uwekezaji wa shughuli za kiuchumi kama vile mahoteli, maduka, shule, hospital na maeneo ya burudani na kadhalika

Mheshimiwa Spika, tano vilevile ni kupunguza migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kuwa, urasimishaji si jibu la kudumu la kuzuia ujenzi holela mijini bali ni utayarishaji wa mipango kabambe ya miji yetu ambayo ikienda sambamba na uimarishaji wa usimamizi na uthibiti wa uendelezaji miji itaweka ustawi mzuri wa mandhari ya nchi yetu na hivyo kufanya nchi yetu kuwa sehemu nzuri ya kuishi.

MHE. SALMA M. MWASSA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza naishukuru Serikali kwa kutambua umuhimu wa urasimishaji, lakini naomba itekeleze kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza migogoro ya ardhi suluhisho muhimu ni kupima, kupanga na kurasimisha na si vinginevyo. Kumekuwa na miradi ya urasimishaji, kwa mfano mradi unaondelea sasa hivi katika Jiji la Dar es Salaam Kimara, mradi ule ni kama umetelekezwa. Wafanyakazi wale hawana hela za kwenda *site*, hawana mafuta na wala hawana vitendea kazi vyovyote katika.

Mheshimiwa Spika, kama hivi ndivyo sasa tuone kwamba kurasimisha inakuwa ni sehemu ya kufanya thamani za ardhi zile kupanda hasa katika Jiji la Dar es Salaam ambako *squatter* sasa hivi katika Jiji la hilo ni tatizo kubwa. Watu wanajenga hovyoyote, mji unachafuka, haupangwi inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, sasa huu mradi uliokuwa *pilot area* kwa ajili ya Dar es Salaam ambao sasa ungeweza kufanya huko kwenye mikoa mingine. Sasa ni kwa nini Serikali haipeleki fedha kwenye mradi ule na kutotelekeza kama ilivyo sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali namba la pili, katika miradi ile ya MKURABITA kwenye urasimishaji huo huo, wananchi walilipa fedha zao huko huko Kimara, wamelipa kati ya shilingi 400,000 mpaka 800,000. Wananchi wale bado wana zile risiti, sasa je, napenda Wizara inahakikishie ni lini hizo hela zitarudishwa kwa wananchi au kuwarasimishia ili waweze kuondokana na hiyo sintofahamu?

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuongozana na mimi kwenda katika hiyo ofisi ya mradi hapo Kimara tuangalie hayo matatizo na mimi kama mtaalamu nimshauri? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Mwassa kwa kufuatilia, lakini vilevile Mheshimiwa Mwassa ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Amekuwa ni mstari wa mbele katika shughuli hizi na pia ni mwanataaluma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba kwa maswali yake mawili aliyoyauliza habari ya kutopeleka fedha katika mradi wa Kimara si kweli. Naomba nisema zoezi la urasimishaji linaloendelea Kimara halijakwama kwa ajili ya pesa, limekwama kwa ajili ya wananchi wengine kutotoa ushirikiano; na hii inatakiwa pia Halmashauri zote kule ambako zoezi hili linafanyika tuwasihani wananchi wetu watoe ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu suala la urasimishaji si la mtaalamu kwenda pale na kuamua nini kifanyike. Anapokwenda katika eneo la mradi ni lazima ashirikishe viongozi waliopo lakini pia wale ambao wanapaka katika yale maeneo yanayofanyiwa urasimishaji. Ikitokea

mmojawapo akagoma au akakataa kukubaliana na kile ambacho kinafanyika zoezi haliwezi kuendelea. Kwa hiyo, mimi niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge tuwasihi wananchi wetu kwa sababu zoezi hili lina manufaa kwao na kwa nchi pia.

Mheshimiwa Spika, swali la pili amezungumzia habari ya MKURABITA, kuhusu habari ya kurudishiwa pesa.

Mheshimiwa Spika, miradi yote iliyoanzishwa na MKURABITA bado inaendelea kufanyika na hii ni kwa sababu tu, kumekuwa na miradi mingi ambayo inaendelea katika maeneo ambapo baadaye MKURABITA walisimama wenyewe, ikiwepo na ile Kusini, walisimama hawakuendelea na hilo zoezi kutokana na tatizo kama hilo hilo la mwanzo ambalo nimelizungumzia.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa wale waliolipa pesa zao hakuna atakayedhulumiwa na wote tutawatambua. Kwa hiyo mimi naomba kama unayo orodha, kwa sababu pale ofisini kwetu hatujawa na orodha, hatujaletewa malalamiko hayo kwa maandishi na kujua kwamba kuna watu wamechangia lakini hawajapewa huduma hiyo. Kwa hiyo mimi nitamwomba Mheshimiwa Mbunge alete orodha hiyo, na Waheshimiwa Wabunge wengine kama kwao kuna watu wenye madai hayo wayalete na ofisi itakuwa tayari kuyashughulikia.

SPIKA: Swali la nyongeza tutaanza na Singida hapa. Mheshimiwa umeamua kukata tamaa?Tutaanza hapo la kwanza, subiri kidogo halafu...

MHE. ALLAN J. KIULA: Nashukuru sana ...

SPIKA: Ngoja kidogo Mheshimiwa. Halafu tutaenda mwisho kabisa pale, halafu tutamalizia mwanzo kabisa hapa. Tuendeleo Mheshimiwa.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuweza kunipatia nafasi ya kuuliza swali.

Kufuatia majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, je, ni lini Wizara itashuka chini kwenye Halmashauri mpya kama vile Mkalama, ikarasimisha maeneo ya wananchi kwa sababu kuna miji midogo inayochipua ambapo wananchi wanahitaji maeneo yao yarasimishwe ili waweze kupata mikopo na ardhi yao iwe na thamani?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kushauri halmashauri mpya zinazoanzishwa, tusikimbillie kwenye suala la urasimishaji, kwa sababu urasimishaji si suluhu ya kupanga miji yetu. Mimi ninachomshauri Mheshimiwa waingie katika maandalizi ya kuwa na mpango kabambe wa kupanga mji wao, ili miji hii yote mipya inayoanza ianze katika mpangilio mzuri wa mipango miji na si kuanza zoezi la kurasimisha. Lakini kwa maeneo ambayo tayari yameshaendelezwa bila kufuata taratibu za mipango miji tutakuwa tayari kushiriki pamoja nao katika kuhakikisha kwamba tunafanya zoezi la urasimishaji, lakini wakati huo huo waingie katika mpango wa maandalizi ya mpango kabambe.

SPIKA: Aah, kumbe Mheshimiwa Kubenea umehama bwana. Eeh, kumbe Mheshimiwa Kubenea umehama kwa hiyo, sikupi nafasi hiyo. (*Kicheko*)

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Spika, linahusu Jimbo la Ubungo.

SPIKA: Sasa kuna watu wawili wamevaa nguo za *blue* wote, wananichanganya. Mheshimiwa pale ndiye uulize swali lako linalofuata. Ni Mhweshimiwa Semesi, nadhani.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, japo nia ya Serikali ni njema kurasimisha ardhi kwenye maeneo ambayo hayajapimwa, lakini kuna *concern* kwamba tunakuwa tunaendeleza *squatters*, maeneo ya wazi ambapo miundombinu inakuja kuwa *challenge*. Sasa badaye mnapotaka ku-*implement*

mambo ya mipango miji au ramani zetu tulizonazo kutakuwa kuna gharama tena husika za kubomolea watu. Je, Serikali nimezingatia hili? Asante.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli anachozungumza nadhani kama nimejibu vizuri, ulinisikiliza wakati najibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Allan, si nia ya Serikali kuona kwamba miji inaendelea kuharibika kwa kuendeleza *squatter* na ndiyo maana nimewaomba Waheshimiwa Wabunge kwa sababu wote ni Wajumbe wa Baraza la Madiwani katika Halmashauri zetu, pale ambapo Serikali imeanza kufanya zoezi la urasimishaji katika maeneo ni jukumu la kila Halmashauri kuhakikisha kwamba wanasimamia maeneo yao ili kusiwe na muendelezo wa ujenzi holela. Kwa sababu zoezi hili linapaswa kusimamiwa na Halmashauri zenyewe husika, Wizara sio rahisi kushuka kila maeneo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli zoezi tunalifanya na inaonekana ni zuri, lakini tusingependa kuona ujenzi holela unaendelezwa. Sasa ujenzi huu utasimama pale ambapo kila halmashauri itawajibika katika eneo lake kuhakikisha inakuwa na michoro ya mipango miji kwenye maeneo yao na kusimamia zoezi la ujenzi holela lisiendelee katika maeneo yao. Tukifanya hivyo, miji yetu itakuwa salama na itakuwa inapendeza.

SPIKA: Mheshimiwa Masoud nilikupa nafasi ya mwisho.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mtulia wa Kinondoni kaniomba sana nimuachie.

SPIKA: Aah, basi, Mheshimiwa Mtulia endelea!
(*Kicheko*)

MHE. MAULID S. A. MTULIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mimi katika maeneo yangu ya Jimbo langu la Kinondoni, hasa Magomeni Mtaa wa Kwa Suna, Hananasifu

Mtaa wa Mkunguni na mitaa mingine, nyumba za wananchi zilifanyiwa urasimishaji, lakini kwa masikitiko makubwa watu wakatumia fursa ile wengine kwenda kukopa. Nasikitika kwamba Serikali imeenda kuvunja nyumba zile bila kulipa fidia kwa wananchi wale.

Je, kwa nini Serikali inavunja nyumba zilizofanyiwa urasimishaji na kupata leseni za makazi bila kulipa fidia?
(Makofi)

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu sana, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, anachokizungumza ni kweli, kuna maeneo yalifanyika hivyo, lakini suala la msingi hapa kupewa leseni ya makazi haina maana ya kwamba pale ambapo utaratibu wa mipango miji umeyapanga vinginevyo yale maeneo hautavunjiwa. Kwa sababu Dar es Salaam yenyewe sasa hivi iko katika mchakato na ninadhani imekamilisha mpango wa *master plan* ya miji ule.

Sasa pale ambapo inaonekana kabisa kwamba kuna suala zima la kutaka kuweka miundombinu inayofaa katika eneo lile watu hawa wanaweza kuvunjiwa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, lakini Wizara ilishatoa tangazo kwa wale ambao walikuwa na umiliki halali na wana hati kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na wamevunjiwa kimakosa, tulisema walete orodha yao na watu wa mipango miji watakwenda kuhakiki waone kweli walivunjiwa kimakosa. Lakini kwa wale ambao waliendelea na ujenzi bila kuzingatia mipango miji imepanga nini katika ule mji hao hawatalipwa na itakuwa ni tatizo. Watu wa Hananasifu na Mkunguni kama alivyosema, kama hao wapo kulingana na maelezo niliyoyatoa, basi tupate wakiwa na hati zao kutoka Wizarani kwetu au kutoka kwenye manispaa inayohusika, tutawa-*consider* kulingana na malalamiko watakavyokuwa wameyaleta.

Na. 57

Ujenzi wa Barabara ya Kilindoni – Utende

MHE. MBARAKA K. DAU aliuliza:-

Ujenzi wa barabara ya Kilindoni - Utende (*Airport Access Road*) yenye urefu wa kilometa 14 umekamilika, lakini mkandarasi CHICO ameijenga barabara hiyo chini ya viwango kwani ina viraka vingi.

Je, ni lini Serikali itaitaka kampuni hiyo kufanya marekebisho makubwa?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kilindoni – Utende ni barabara inayounganisha kiwanja cha ndege cha Mafia na sehemu muhimu za kiuchumi, yakiwemo maeneo ya kitalii ya Fukwe za Utende na Gati la Kilindoni.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kilindoni – Utende yenye urefu wa kilometa 14 ilijengwa kwa kiwango cha lami na Kampuni ya *China Henan International Cooperation Group Limited (CHICO)* na kukamilika tarehe 1 Januari, 2015 na kufuatiwa na kipindi cha uangalizi cha mwaka mmoja hadi tarehe 1 Januari, 2016.

Hata hivyo, Wizara kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) ilikataa kuipokea barabara hiyo kutokana na kasoro zilizojitokeza wakati wa kipindi cha uangalizi na iliamuliwa ufanyike uchunguzi, ili kubaini kiwango cha mapungufu ya ubora katika ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchunguzi yalionesha kuwa baadhi ya sehemu za barabara ya Kilindoni – Utende hazikujengwa katika ubora unaotakiwa, hivyo mkandarasi ameelekezwa kurudia kwa gharama zake mwenyewe maeneo yote yaliyoonekana kuwa na mapungufu kulingana na matakwa ya mkataba; kazi hiyo itaanza mara baada ya kipindi cha mvua kumalizika.

Aidha, uangalizi wa karibu wa maeneo mengine unaendelea kufanywa na *TANROADS* ili kuhakikisha kuwa barabara hiyo inakabidhiwa Serikalini ikiwa na viwango vya ubora vinavyokubalika kimkataba.

SPIKA: Waheshimiwa mnatoka Mafia? Mheshimiwa Dau, swali la nyongeza. (*Kicheko*)

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwanza Naibu Waziri anakiri kwamba barabara ile imejengwa chini ya kiwango; lakini Naibu Waziri atakubaliana na mimi, alipotembelea Mafia tuliikagua barabara hii mimi na yeye. Barabara hii si ya kufanyiwa matengenezo makubwa, ni ya kurudiwa upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ng'ombe akikatisha kwenye barabara anaacha mashimo, barabara ya lami! Gari likipata *puncture* ukipiga jeki, jeki inakwenda chini kama unapiga jeki kwenye tope, kule Mafia wanaita barabara ya *big G* (*chewing gum*).

Mheshimiwa Spika, sasa nina maswali mawili. Swali la kwanza; kwa kuwa Serikali inakiri kwamba mkandarasi huyu ameijenga chini ya kiwango, ni hatua gani za kimkataba na za kisheria zimechukuliwa dhidi ya huyu mkandarasi aliyeisababishia Serikali hasara? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wananchi wa maeneo ya Kilindoni, Kiegeyani na Utende ambao walikuwa ni

wahanga wa kubomolewa nyumba zao, wengine wamekatiwa minazi yao na mikorosho yao na mazao yao mbalimbali, mpaka leo wengi wao hawajalipwa fidia kutokana na ujenzi wa barabara ile, ningependa nisikie kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, nini hatma ya waathirika hawa wa fidia? Ahsante.

SPIKA: Hii barabara hii ya Kilindoni – Utende yaani mbwa akipita tu anaacha *foot prints!* Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer* Edwin Ngonyani, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kwamba nilikuwa Mafia na Mheshimiwa Dau na tuliikagua hiyo barabara. Lakini namuomba tu asiongeze utani sana ndani ya Bunge, maeneo machafu ni machache ambayo yameshaainishwa na kwa mujibu wa mkataba tumeshachukua hatua ya kumlazimisha mkandarasi kurudia maeneo hayo kwa gharama zake.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu fidia; nimuombe Mheshimiwa Kitwana Dau, kwamba yale tuliyoongea Mafia ayazingatie. Nikuhakikishie yeyote mwenye haki ya kulipwa fidia atalipwa. Sehemu ya wengi tunaowaongelea pale ni wale ambao waliifuata barabara.

SPIKA: Mheshimiwa Profesa Maji Marefu nimekuona, Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Riziki Mngwali

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona, lakini vilevile niipongeze sana Wizara hii.

Katika Serikali ya Awamu ya Nne kupitia Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi iliweka ahadi kwamba itaweka lami barabara ya kutoka Korogwe - Kwa Shemshi - Dindila - Bumbuli hadi Soni, lakini mpaka leo hii hakuna ufafanuzi wowote wa kujengwa kwa lami. Nataka Serikali iwahakikishie wananchi kule kwamba barabara ile ni lini sasa itajengwa kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa, hilo si lingesubiri bajeti ya Wizara? Majibu kwa ufupi Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, hii barabara anayoizungumzia ya kuanzia Korogwe kuelekea Bumbuli – Dindila mpaka kule mwisho ni barabara ambayo amekuwa akiiongelea mara nyingi kuanzia kipindi cha bajeti ya mwaka jana. Nimhakikishie tu yale ambayo tulimueleza, kwamba barabara hii kwanza itaanza kujengwa kutokea Korogwe, kama ambavyo usanifu ulionesha.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, nimhakikishie kwamba haya anayoyasikia kuhusu hii barabara sio kweli. Serikali ina dhamira ya dhiti ya kutekeleza ahadi yake ya kujenga hii barabara kwa lami. Kama nilivyomueleza mara nyingi tu ofisini na maeneo mengine na hata alipomuona Waziri wangu, nikupongeze sana kwa namna unavyofuatilia kwamba barabara hii tutajenga baada ya kukamilisha hizi barabara ambazo sasa hivi zinatuletea madeni mengi, tunataka tuziondoe kwanza hizo ili tuzianze hizi nyingine, lakini kimsingi katika miaka hii mitano ahadi hiyo tutaitekeleza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na wakandarasi kujenga barabara chini ya kiwango au kukarabati barabara chini ya kiwango si jambo geni na Mheshimiwa Spika, na wewe ni shahidi barabara ya kutoka Morogoro kuja hapa Dodoma sasa hivi tayari imeshavimba, Wabunge wote mnajua. Lakini hiyo barabara ninayoitaja pia inapita Jimboni kwako, nadhani shahidi tayari sasahivi imeshaanza kuvimba, nimeona tu nikuulizie boshi wangu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge pia mashahidi, ukarabati unaofanywa hata kwenye barabara za hapa Dodoma, *Area D*, *Area C* pia uko chini ya kiwango, unaigharimu sana Serikali kuwa tunakarabati barabara mara

kwa mara pindi Waheshimiwa Wabunge wanapokuja Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kingine, barabara ya kutoka Musoma – Bunda na yenyewe pia, ilishaharibika kabla hata ya kukabidhiwa.

Swali langu, je, mna mkakati gani katika barabara mpya ya kutoka Kisorya - Bunda Mjini - Nyamswa, ambayo bado haijajengwa, inajengwa kwa kiwango cha lami, ili barabara hiyo isiigharimu Serikali fedha za kutosha na iwe ya kiwango? Naomba jibu zuri na ujue unamjibu Waziri Kivuli na Mjumbe wa Kamati Kuu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, nimechanganyikiwa kwa sababu swali ninalotakiwa nilijibu ni moja, sijui ni jibu lile la Mbande, niache lile la Kisorya au nijibu la Kisorya niache haya ya Mbande?

SPIKA: Nimekuachia kama *Engineer* nikajua tu utapata moja la kujibu hapo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Morogoro hadi Dodoma na viunga vya Dodoma huwa zinajengwa kwa kufuata mikataba. Katika ile mikataba kuna viwango ambavyo vinawekwa kwa mkataba na kutokana na kiwango cha fedha. Kwa hiyo, mimi nimhakikishie Mheshimiwa Ester Bulaya kwamba barabara hizi za kutoka Morogoro hadi Dodoma, pamoja na Dodoma Mjini, tunahakikisha kwamba kile kiwango cha mkataba kinafikiwa. Nichukue nafasi hiyo kuwapongeza watu wa *TANROADS* kwa kuhakikisha kwamba wanasimamia kwa kiwango kikubwa na pale inapotokea mkandarasi aliyetengeneza hajafikia kiwango, hatua bhuwa zinachukuliwa.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hii barabara ambayo Mheshimiwa Dau ameisema, wenzenu ndiyo ilikuwa lami ya kwanza tumeiona katika miaka 50 ya uhuru, kwa hiyo, ilipoharibika baada ya siku chache kwa kweli tumeumia. Sasa hii barabara ukitoka pale *round about* ya Kilindoni kwenda Utende ni kwamba zaidi ya theluthi mbili ya barabara ni mbovu. Sasa nashangaa Mheshimiwa Naibu Waziri anavyotwambia kwamba ni sehemu chache.

Sasa swali langu, je, Mheshimiwa Waziri atatuhakikishia ushirikishwaji uliokamili wa wadau wote wa Mafia na watumiaji wa barabara ile kabla ya hiyo kazi ya kuanza ukarabati ili na sisi tujue hilo andiko mliosema ninyi mapungufu machache na kazi itafanyika kwa kiasi gani? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, nakubali, tutashirikisha wadau na kwa taarifa hii *TANROADS* Mkoa wa Pwani wawashirikishe wadau wa Mafia kabla *CHICO* hajaanza kurekebisha yale maeneo ambayo yamegundulika yana matatizo.

SPIKA: Ahsante sana, tunaendelea Wizara hiyo hiyo bado tunayo. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe.

Na. 58

**TBA Kujenga Ofisi na Makazi ya Mkuu
wa Wilaya ya Mbogwe**

MHE. AUGUSTINO M. MASELE aliuliza:-

Wakala wa Majengo Tanzania (*TBA*) walipewa kandarasi ya kujenga Ofisi na Makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe lakini ujenzi huo umesimama.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza tena ujenzi huo na kuukamilisha kupitia *TBA*?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilitenga fedha kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa nyumba 149 za viongozi katika maeneo mapya ya utawala katika mikoa 20 ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, mradi ulihusisha ujenzi wa nyumba za Wakuu wa Mikoa nne, Wakuu wa Wilaya 21, Makatibu Tawala wa Mikoa nyumba nne, Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa nyumba 40, Makatibu Tawala wa Wilaya nyumba 38 na Maafisa Waandamizi nyumba 42.

Mheshimiwa Spika, mkataba wa ujenzi wa nyumba 149 za TAMISEMI ulitiwa saina tarehe 3 Mei, 2014 kati ya Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kwa gharama ya shilingi 17,988,016,924.56. Hadi mradi unasimama kiasi cha shilingi 4,169,477,121.62 sawa na asilimia 23.2 kilikuwa kimetolewa kwa ajili ya ujenzi kwa gharama hizo. Kiasi hicho cha fedha kiliwezesha kuanza ujenzi wa nyumba 84 kati ya nyumba 149 za miradi.

Katika Wilaya ya Mbogwe mradi ulihusisha ujenzi wa nyumba nne, zikiwemo nyumba moja ya Mkuu wa Wilaya, nyumba moja ya Katibu Tawala na nyumba mbili za Maafisa Waandamizi kwa gharama ya jumla ya shilingi 500,585,277.70. Ujenzi wa nyumba hizi kama zilivyo nyumba nyingine chini ya mradi huu umesimama kutokana na ukosefu wa fedha. Mradi huu umepangwa kuendelea kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2017/2018.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali hata hivyo nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kupitia kwa Naibu Waziri imekiri kwamba ni asilimia 23 tu ya zoezi zima la ujenzi wa nyumba za Wakuu wa Wilaya na Mikoa ndizo zilizokuwa zimetetelezwa. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha kwamba hizi nyumba zinakamilika kwa wakati katika mwaka wa fedha ujao?

(b) Je, Serikali imepanga kiasi gani cha fedha kwa Wilaya ya Mbogwe katika mwaka ujao wa fedha? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la swali la msingi kwamba kuna kiwango cha fedha ambazo *TBA* wanahitaji kuzipata ili waweze kukamilisha zoezi hili la ujenzi. Naomba tu kama nilivyosema kwamba fedha zimetengwa katika mwaka huu wa 2017/2018 na niombe radhi sina kile kiwango kamili kilichotengwa chini ya TAMISEMI tutaweza kukupa hizo taarifa baadaye baada ya kuwasiliana na watu wa TAMISEMI kujua kiasi gani kimetengwa. Lakini nina uhakika na nimepata taarifa kutoka *TBA* kwamba mwaka huu wa fedha unaokuja wanaanza kujenga nyumba hizo hadi kuzikamilisha kwa sababu wameahidiwa kupata fedha zilizobakia zote.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Sixtusi Mapunda kwa upande wa CCM na upande wa CHADEMA basi Mheshimiwa Pauline Gekul utawakilisha. Tuanze na Mheshimiwa Sixtus Mapunda.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo linaloikabili Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe linafanana na linaloikabili Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, lakini tofauti iliyoko kati ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe na ile ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbinga imekwishakujengwa takribani zaidi ya miaka mitano iliyopita, imekwisha kuezekwa, isipokuwa mpaka sasa haijamalizika kwa kutopakwa rangi, haijawekwa madirisha,

haijawekwa mfumo wa *wiring* pamoja na milango na madirisha ambapo thamani ya umaliziaji huo inakadiriwa kuwa 300,000,000. Waziri anawahakikishiaje wananchi wa Wilaya ya Mbinga kwamba mwaka huu hautaisha mpaka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbinga inakamilika? Kwa sababu inapozidi kukaa zaidi ya miaka mitano inazidi kupoteza ubora, inakuwa ni nyumba ya popo, bundi na kadhalika ambayo siyo malengo ya ujenzi wa ile ofisi? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilijibu swali la msingi, na bahati nzuri nyumba anayoongelea ina uhusiano wa moja kwa moja na swali la msingi, kwamba mwaka ujao wa fedha 2017/2018 *TBA* imeahidiwa kupata fedha kutosha na itakamilisha majengo ambayo imeyaanza. Aidha, nikupongeze, maana sikutengemea utarudia tena kuliuliza hapa wakati ulishakuja ofisini na tukaongea kwa kirefu. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri ukiona swali la nyongeza au swali msingi linaulizwa hapa siyo kwamba Mbunge hajui anataka wananchi wake wasikie kuhusu hicho kitu. Kwa hiyo, hata kama uliongea na Mbunge lazima aulize tena hapa ili kama ulikuwa unaongea ya ukweli basi uwaambie wananchi wasikie. Mheshimiwa Pauline Gekul swali la mwisho kwenye eneo hilo. (*Makofi*)

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni *TBA* walikabidhiwa maeneo ambayo yalikuwa ya *National Housing* ambayo yalikuwa katika Halmashauri zetu ili waweze kufanya ujenzi mbalimbali. Lakini kwa bahati mbaya maeneo haya ambayo *TBA* wamekabidhiwa yaliyokuwa tayari yanatumika na Halmashauri zetu, mfano ni eneo la *National Housing* lililoko pale Mji wa Babati ambalo linatumika na vijana wetu wa Machinga. Ombi hilo tulishapeleka Waziri ya Ardhi, lakini sasa maeneo yale yamekabidhiwa *TBA* ambayo iko Wizara ya Ujenzi.

Naomba nifahamu Serikali au Wizara ya Ujenzi iko tayari na *TBA* kupokesa maombi yetu tena ili eneo hilo la *National Housing* libaki kwa vijana wetu wa Machinga wasisumbuliwe kama ambavyo kauli ya Rais imesema?

SPIKA: Hilo kweli ni la Uchukuzi au ni la Ardhi ambao ndio wenye *National Housing*?

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, la *TBA*.

SPIKA: La *TBA*?

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, ndiyo.

SPIKA: Haya Mheshimiwa Naibu Waziri kama hilo jambo unalifahamu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iko tayari kupokea hayo maombi kama ambavyo umesema na tutayaangalia kwa maslahi mapana ya nchi. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushuru sana, Wizara ya mwisho kwa siku ya leo ni Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, anauliza kuhusu umeme kukatikakatika Mheshimiwa Lucy Owenya.

Na. 59

Tatizo la Kukatika Umeme - Manispaa ya Moshi

MHE. LUCY F. OWENYA aliuliza:-

Halmashauri ya Manispaa ya Moshi imekuwa na tatizo la kukatika umeme mara kwa mara.

(a) Je, ni sababu zipi zinazosababisha hali hiyo?

(b) Je, ni lini tatizo hili litakwisha?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, naamini kabisa jambo hilo linawagusa Waheshimiwa Wabunge wengi Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Medard Kalemani.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kilimanjaro ni miongoni mwa mikoa inayofaidika na utekelezaji hali ya utekelezaji wa miradi ya *TEDAP*. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia na unalenga kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme nchini. Kazi za mradi huu kwa Mkoa wa Kilimanjaro zinajumuisha kuongeza uwezo wa vituo viwili vya kupoza umeme vya *Trade School* kutoka *MVA 5* hadi *MVA 15*. Pia kuboresha miundombinu hiyo katika maeneo ya Boma Mbuzi kutoka *MVA 10* hadi *MVA 15*. Hali kadhalika kubadilisha waya katika njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 kutoka milimita 100 hadi milimita 150. Vilevile kuongeza uwezo wa kusafirisha umeme muhimu na bora.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulianza kutekelezwa mwezi Januari, 2014 na umekamilika kwa asilimia 95 ambapo sasa kilometa 50.95 kati ya kilometa 54.63 zimeshajengwa na waya zimeshaunganishwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha utekelezaji wa mradi huu kumekuwa na ulazima wa kuzia umeme katika baadhi ya maeneo ili kupisha marekebisho maalum na kwa usalama zaidi. Zoezi hili limekuwa likifanyika kwa kutoa taarifa katika vyombo mbalimbali vya habari. Tatizo la kukatikatika kwa umeme katika maeneo ya Halmashauri ya Mji wa Moshi litaisha mara baada ya shughuli za Mradi huu kukamilika mwezi Mei, 2017.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri naomba uangalie, uzunguke ikupe picha ya tatizo la kukatikatika kwa umeme

Ilivyo kubwa. Sina namna hata ya kujua nani sasa apate nafasi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Lucy Owenya, halafu tutaona tunafanyaje sasa hapo. Swali la nyongeza Mheshimiwa Lucy Owenya kwa kuanzia na wengine nitawaangalia baada ya hapo, nimeshawaona ona kiasi. (*Kicheko*)

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kunipa majibu yenye matumaini.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kukatika kwa umeme limeleta madhara makubwa sana kwa wateja. Watu wamekuwa wakiunguliwa nyumba zao wengine vifaa ndani ya nyumba vikiungua kama friji, *television* na kadhalika. Tatizo la hitilafu ya kukatikakatika kwa umeme na kuunguza vifaa vya wateja si tatizo la mteja, ni tatizo la *TANESCO*. Nataka kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ni lini sasa *TANESCO* itaanza kufidia wananchi kwa kuunguliwa na vitu kwa sababu siyo tatizo lao, kama ilivyo kwenye nchi za Ulaya ambako huwa wanafidia wananchi wakati matatizo yakitokea na kupata hitilafu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Sasa hivi tunakwenda katika Tanzania ya viwanda, na Mheshimiwa Waziri amesema Kilimanjaro tutakuwa na umeme wa uhakika. Nataka nijue na uwahakikishie wananchi wa Kilimanjaro, je, umeme huu utaweza kutosheleza kwa wafanyakazi na wafanyabiashara wa Mkoa wa Kilimanjaro ambao wanataka kuwekeza katika viwanda? Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Profesa majibu.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza niongee tatizo la kukatikakatika umeme. Waheshimiwa Wabunge njia nyingi za umeme nchini ni zile ambazo *TANESCO* ilianza nazo mwaka 1964. Hata mimi kwetu

Musoma Mjini umeme ulikuja mwaka 1967, hata pale kwetu hazijabadilika. Sasa ni uamuzi wetu, tuamue kuwa na uvumilivu tuzime tutengeneze au tuendeleo na matatizo uwe unawaka unakatikatika. Kwa hiyo, nadhani jibu zuri ni kwamba tuvumilie miundombinu ni ya zamani na tunairekebisha, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala ambalo Mheshimiwa Mbunge amesema *TANESCO* ina taratibu za kutoa fidia ikiwa kama vyombo vimeharibika na kosa ni la umeme, kosa ambalo ni la *TANESCO*, wana taratibu zao unapeleka madai unajaza fomu wanafanya tathmini, huo utaratibu upo.

Sasa niongelee hili la kukatikatika kwa ujumla lingine la umeme wa uhakika. Kilimanjaro kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba inawekwa miundombinu mipya halafu Kilimanjaro na Arusha kuna *sub station* tutakwenda kuifungua ya *KIA* ambayo ni mpya, umeme umeongezeka pale tumeweka *substation*. Lakini isitoshe ni kwamba tunaongeza umeme wa msongo mkubwa. Hii Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wanaonisikiliza ni kwamba njia za kusafirishia umeme nchini zilikuwa za *KV 220*, sasa hivi tunaweka *440*, ni karibu mara mbili.

Kwa hiyo, njia ya kutoka Iringa, Dodoma kwenda mpaka Shinyanga tayari, ndiyo maana siku hizi umeme haukatikatikati kwa sababu tuna umeme mwingine unasafirishwa humu, na uwezo wake unaweza ukachukua mpaka *MW5000* kutoka Iringa kwenda Shinyanga. Kwa hiyo, inabidi tujaze mle umeme ni kama ambavyo unajaza maji zaidi kwenye bomba, kwa hiyo, umeme mwingi unakuja.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kaskazini tunajenga *transmission line* mpaka kutoka Singida kwenda Namanga ambayo nayo ni ya *kilovolts 400*; itachukua huo umeme. Juzi nilikuwa naongea na mkandarasi anataka kujenga *transmission line* ya kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma.

Ndugu zangu wa pembeni mwa Ziwa Tanganyika, tunakamilisha majadiliano ya njia kubwa ya umeme kutoka Iringa, Sumbawanga, Mpanda, Kigoma na Nyakanazi. Kuna ambayo imeshaanza kujengwa na Balozi anataka akaizindue ya kutoka Makambako kwenda Songea kusudi Songea iwe kwenye Gridi ya Taifa. Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote hii nchi ya viwanda itajengwa na Wizara ya Nishati na Madini, ndiyo yenye uwezo wa kuijenga msiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

SPIKA: Kwa kweli nikitoa swali la nyongeza nitakuwa sijatenda haki jinsi Wabunge mlivyo wengi mlivyosimama, naomba niwanyime swali la nyongeza wote kabisa na muda wetu pia umeisha, nawashukuruni sana. Hiyo inampa picha profesa pamoja na majibu yake mazuri kwamba kazi za kufanya bado ni kubwa na swali la msingi ni kwamba *TANESCO* hii hii kweli itaweza kumaliza matatizo haya hivi ilivyo leo? Maana hii ni dalili kwamba liko tatizo kubwa sana.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo, la kwanza la wageni, kwenye Jukwaa la Spika, nina mgeni ambaye ni Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* Profesa Mussa Assad. Profesa Mussa Assad karibu sana. Ameambatana na watoto wake watatu pamoja na Maofisi kutoka Ofisi ya *CAG*. Karibuni sana naomba wote msimame. Karibuni sana. Tungependa kuchukua hii sisi kama Bunge kukupongeza sana *CAG* kwa kazi nzuri sana ambayo unaifanya kwa nchi yetu. Tunakutia moyo na tunaahidi ushirikiano wa karibu sana na wewe kwa kadri utakavyoona inafaa na sisi tuko tayari, karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna Waheshimiwa Wabunge walikuwa wamekubaliana kukutana na Mheshimiwa Kangi Lugola hapo nje mara tu baada ya kumaliza shughuli hizi sasa ameahirisha jambo hilo anaomba mkutane naye baada ya likizo hii fupi ya Pasaka.

Waheshimiwa Wabunge, tuna taarifa muhimu sana kuhusu ratiba ya mazishi ya Mheshimiwa Dkt. Elly Marko Macha, nayo itakuwa kama ifuatavyo:-

Naomba kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba taratibu zote za kule Uingereza za kumrudisha ndugu yetu Marehemu Dkt. Elly Macha sasa zimekamilika. Kule kuna taratibu nyingi za kisheria na kadhalika, haikuwa rahisi kuharakisha mchakato huo na tunashukuru sana Ubalozi wetu nchini Uingereza ambao umesimamia sana jambo hili. *(Makofi)*

Kwa jinsi hiyo, mwili wa Mheshimiwa Dkt. Elly Marko Macha unatarajia kuwasili nchini Tanzania Alhamisi ya wiki ijayo, tarehe 20 Aprili, 2017 katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Jijini Dar es Salaam, tarehe 20 Aprili saa 9.00 alasiri kupitia ndege ya Shirika la Emirates. Baada ya mwili kuwasili utapelekwa na kwenda kuhifadhiwa katika Hospitali ya Jeshi ya Lugalo. Siku inayofuata tarehe 21 ambayo ni siku ya Ijumaa mwili utasafirishwa kutoka Jijini Dar es Salaam na kuja hapa Dodoma na utaletwa katika viwanja vya Bunge ambapo kutakuwa na ibada fupi, salaam za rambirambi na baadaye Waheshimiwa Wabunge na viongozi wengine mtakaokuwepo mtapata nafasi ya kutoa heshima zenu za mwisho kulingana na itifaki.

Siku hiyo tarehe 21 Aprili alasiri mwili wa Marehemu utasafirishwa kuelekea nyumbani kwake Mkoa Arusha ambako pia kutakuwa na ibada ya kuaga mwili wa marehemu kwa viongozi wengine wa kitaifa wa Mkoa na wananchi wa Arusha na familia kwa ujumla. Zoezi lote hilo litafanyika nyumbani kwake kule Arusha.

Waheshimiwa Wabunge, siku ya Jumamosi tarehe 22 Aprili, asubuhi mwili wa Marehemu Dkt. Macha utasafirishwa kutoka pale nyumbani kwake Usa River Mkoa Arusha kuelekea nyumbani kwa wazazi wake Kirua Vunjo, Wilaya Moshi Mkoa Kilimanjaro kwa mazishi.

Waheshimiwa Wabunge, taarifa zaidi ikiwa ni pamoja na ratiba nzima ya mazishi tutaendelea kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge kadri siku zinavyosonga mbele.

Basi baada hatua hii tulipofikia leo tusiwe na mwongozo wala nini, leo tulikutana hapa pamoja na mambo mengine kuweka mambo sawa sawa ili Pasaka hii isiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

Natambua kabisa Waheshimiwa Wabunge, wengi mtakuwa mnasafiri kwenda sehemu mbalimbali za nchi yetu kwa ajili ya mapumziko mafupi ya Pasaka, na jinsi hali ilivyo ngumu najua kabisa wengi wenu mnapanda mabasi na mabasi haya ya Dodoma mengi yanaondoka saa tano na kitu. Kwa hiyo ni vizuri kabisa tuagane mapema ili muweze kuwahi *stand*. Nawaombea sana safari njema ya amani na salama. Nawaomba madereva wote wajue wamebeba Waheshimiwa huko kwenye mabasi yao kwa hiyo waende taratibu. Tutakutana tena wiki ijayo baada ya sikukuu hii ya Pasaka kuwa imeisha. *(Makofi)*

Ninawatakia kila la kheri ninyi na wapiga kura wenu wote na pia kwa niaba ya Bunge tunawatakia kila la kheri Watanzania wote na kheri ya Pasaka popote pale watakapokuwa. *(Makofi)*

Baada ya maneno hayo Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa niaharishe shughuli za Bunge hadi siku ya Jumanne, tarehe 18 Aprili, 2017 Saa Tatu Asubuhi.

(Saa 4.20 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 18 Aprili, 2017 Saa Tatu Asubuhi)